B. Rum. 7:4, 6, Paulo alisema tumekufa kwa zile sheria ambazo zilifundisha kutamani ni dhambi, ziliandikwa katika torati. Sasa ni wapi kwenye torati zimeandikwa kutamani ni dhambi. Ni kwenye Amri Kumi, katika kitabu cha Kutoka 20, tunaona Mungu alitoa amri kumi hapa na katika mstari wa 17 aliwaambia Waisraeli wasitamani. Pia ukiangalia kitaka cha Kumbukumbu la Torati tunaona tena Musa anarudia zile Amri Kumi na katika sura ya 5 na mstari wa 21, tunaona tena Mungu aliaandika tusitamani. Sasa Paulo alisema asingejua kutamani ni dhambi pasipo torati, ni wapi kwenye torati kuliandikwa tusitamini? Kwenye sehemu zilioorodheshwa Amri Kumi. Na Paulo <u>alisema tumekufa kwa ile sheria!</u> Kwa ile sheria inaongea kuhusu kutamani tumekufa! Na ile sheria pia inasema tushike sabato!

B. Tena katika Hos. 2:11 nabii Hosea alitabiri kwamba Mungu ataiondoa sabato, "Tena nitaikomeshea furaha yake yote, na sikukuu zake, na siku zake za mwanadamo wa mwezi, na ___________ zake, na makusanyiko yake yote yaliyoamriwa."

C. Kwa hiyo kama tunataka mauti basi tufuate vipande viwili vya mawe. Kwa sababu Mungu alisema atakomesha sabato na Paulo alisema tumekufa kwa ile sheria na tena alisema yale mawe yana huduma ya mauti.

II. Tena Wasabato wanafundisha Amri Kumi zilitolewa kwa watu wote.

A. Katika Nehemia 9:14, tunaona lini amri kumi zilitolewa. "Ukawajulisha sabato yako takatifu, na kuwaagiza maagizo, na amri, na sheria, kwa mkono wa mtumishi wako, ____________."
   1. Amri Kumi zilitolewa wakati Musa alikuwa hai.

B. Katika Nehemia 9:13, tunaona wapi amri kumi zilitolewa. "Tena ulishuka juu ya mlima ____________, ukasema _________ toka mbinguni, ukawapa hukumu za haki, na sheria za kweli, na amri nzuri na maagizo."
   1. Amri Kumi zilitolewa kule mlima Sinai.
   2. Na mstari wa 13 inasema "ukasema nao", "Nao" ni wakina nani?
   3. Nao ni wana Waisraeli!
   4. Amri Kumi zilitolewa kwa wana Waisraeli walitoka Misri na kuendelea. Siyo kwa Baba zao wa zamani.

C. Kwa nini Amri Kumi zilitolea kati ya Mungu na wana WaIsraeli? Tukisoma Kut. 31:17 tunaona ni

kati ya Mungu na wana Waisraeli kwa milele.

III. Wasabato wanadai Kanisa la Katoliki walibadirisha siku ya ibada iwe Jumapili na sio Jumamosi.

A. Hapa sio kweli. Kanisa la Katoliki lilianza mwaka wa 325 bk. Na kuna maandishi ya kihistoria ya kutosha ya kuonyesha watu wa Mungu walikuwa na sali Jumapili. Kanisa la Katoliki walichofanya ni kuifanya Jumapili iwe kama sikukuu. Na hata utawala wa Rumi walifanya haya pia. Lakini watu wa Mungu walikuwa wanafanya ibada siku ya Jumapili toka siku ya Pentokosti, Mdo. 20:7.

B. Ignatius aliandika katika <u>Magnesians 9:1</u>, alisema katika mwaka wa 108 bk., "Wale waliotembea katika mapokea ya zamani walipokea tumaini jipya na waliaacha kuishika sabato, lakini sasa wanaishi kwa siku ya Bwana ilitokeo hivyo kupitia Yeye na mauti yake."

C. Justin Martyr aliandika tena katika mwaka wa 140 bk, "Katika siku inayoitwa Jumapili watu wote wanaoishi mijiini, au vijijini, walikusanyika katika mahahli pamoja, na ukumbusho wa mitume na manabii walifundisha, na kama muda ulikuwepo.....walichukuwa mkate na divai.....matajiri kati yetu wanasaidia wanaohitaji."

D. Na kuna maandishi mengi tu yanaonesha kwamba Kanisa la Kwanza la Kristo lilifanya ibada siku ya Jumapili.

IV. Wasabato wanadai Yesu alianza kuiondoa dhambi katika siku ya 22/10/1844, wakati alipoingia katika Patakatifu pa Patakatifu kule mbinguni.

A. Wanasema haya kwa sababu mwanzilishi wao alidai kwamba Yesu atarudi siku ile lakini Yesu hakufa kwa hiyo wanatengeneza mafundisho bila msingi toka maandiko.

1. William Miller alitabiri Yesu atarudi siku ile, kwa sababu Yesu hakufika ina maana William Miller ni mwalimu wa uongo, soma Kumb. 18:22.

B. Yesu ameishaa tengeneza upatanisho kwetu sisi toka karne ya kwanza, somo Ebr. 9:11-14.

C. Na kazi yake <u>alimaliza</u> wakati alipaa kurudi mbinguni, Ebr. 1:3.

D. Njia ya kuiondoa dhambi ilianzaa katika karne ya kwanza, "lakini sasa, mara moja tu, katika _______________ wa nyakati, ________________, __________________ dhambi kwa dhabihu ya nafsi yake."

1. Kwa hiyo kule msalabani dhambi zilianza kuondolewa. Siyo katika mwaka wa 1844.

E. Yesu aliingia Patakatifu pa Patakatifu wakati alipopaa kurudi kwa Baba kabla ya siku ya Pentokosti. Na aliingia kwa Baba ili awaombee. Ebr. 9:24; 7:25; Rum. 8:34.

1. Yesu hakuingia ili asamehe dhambi, dhambi zetu zinasafishwa kupitia mauti yake. Rum. 6:3-5.

F. Kwa hiyo wazo la kuwa Yesu aliaanza kusamehe au kuiondoa dhambi katika mwaka wa 1844 ni uongo!

1. Soma Mdo. 2:28; 1 Pet. 3:21 na Rum. 6:3-4.

IV. Wasabato wanatawaza miguu kabla ya kuchukua meza ya Bwana.

A. Ukisoma Luka 22 na Yoh. 13 utasoma kuhusu tendo la kutawaza miguu.

1. Kwanza, katika Yoh. 13 haikuwa siku ya ibada siku ile.

2. Pili, Yesu alitawaza miguu ya wanafunzi <u>baada</u> ya meza yake.

3. Tatu, kama ni sheria na ni lazima tutawaze miguu. Na kama tutahukumiwa kwa sababu hatutawazi miguu? Basi, nani alitawaza miguu ya Yesu? Hakuna Mtu!

4. Kielelezo Yesu aliacha hapa ni kuwa mnyenyekevu, kwa sababu ukiangalia Lk. 22 unaona mitume walikuwa wana bishana nani mkubwa zaidi na nani atachukua nafasi ya Yesu. Sasa Yesu alifundisha katika Yoh. 13 kwamba mtumishi ndio bora katika ufalme wake.

5. Tena sheria ya Yesu aliweka katika Yoh. 13 iko kwenye mstari wa 34.

Hitimisho:

Tumeona tena kwamba Wasabato ni dini iliyoanzishwa na mwongo. Alikuwa ana tabiri na alishindwa halafu akaanza kutengeneza mafundisho ili asionekana mjinga mbele ya watu. Yesu katika karne ya kwanza alishaingia kwa Baba. Alikua ana kaa pamoja na Baba. Tena hakuna hata mstari mmoja kwenye maandiko unaeleza ya kuwa Yesu atasubili miaka 1811 ili aingie kwa Baba. Jamani muda umefika tusidanganywe na watu siku hizi. Wote tunauwezo wa kununuwa Biblia na wote tunauwezo wa kusoma na kuandika. Basi tufanye, ili tuchunguze mafundisho ya watu.

**Somo La Ishirini** **Jina ______________**

## Mafundisho Ya Madhehebu

**(Sehemu ya Tatu)**

Kwa majuma mawili tutajifunza kuhusu Mashahidi wa Yehova. Tutaangalia kuhusu historia yao pamaja na mafundisho yao. Halafu tutaangalia katika kila kipengele Biblia inasemaje.

**Historia kwa Ufupi:**

Charles Taze Russell wa Marekani alianza kufundisha watu kwamba Yesu ya karibu kusimamisha ufalme wake hapa ulimwenguni. Katika mwaka wa 1872 bk. wafuasi wake waliunda chama cha ushirika. Lakini chama hakikuitwa Mashahidi ya Yehova mpaka mwaka wa 1931.

Charles Russell, mwanzilishi wao tena alichukua cheo cha juu katika Mashahidi na alikuwa anaitwa "Rais". Lakini baada ya kifo chake katika mwaka wa 1916 walimchagua Joseph Rutherford awe rais wao wa pili. Kazi ya rais ni sawa na Papa katika madhehebu ya Katoliki. Rais wao ni mkubwa wa dhehebu hayo na ni mkuu wa Watch Tower na Tract Society.

Rutherford alikufa katika mwaka wa 1942 na N. H. Nkorr alichaguliwa awe rais katika mwaka 1942. Katika mwaka wa 1950 waliandika tafsiri yao ya Biblia inayoitwa "New World Translation". Na kila miaka kadhaa wanafanya upya tafsiri hiyo ili wabadirisha mistari ili mistari ifuatane na mafundisho yao.

**Wanzilishi na Matatizo wao:**

Charles Taze Russell, alikuwa Marekani. Pia alikuwa mwanzilishi wao. Na aliandika vitabu sita vinavyoitwa "Mafunzo Ndani ya Maandiko".

Charles Russell kwa sisi Wamarekani tunafahamu sana. Na tunafahamu kama mzinzi, mwongo na alikuwa Mhuni sana. Katika kitabu cha "Churches of Today" uk. 97, tunaambiwa yafuatayo:
"Alipelekwa mahakamani na mkewe akishitakiwa kuwa ni mzinzi! Mahakamani, alikiri mwenyewe kwamba **alikuwa na wapenzi wengi.** Basi, serikali iliamua kuwa ni haki kwa mke apewe talaka na kumwacha. Tena, serikali ilimwamru Russell ampe mkewe fidia. Russell alidai kuwa hana fedha. Lakini, serikali ilipeleleza mamabo yake ikagundua kuwa likuwa na fedha za Marekani $317,000 ambazo alikuwa amezificha kwa ujanja! Hivyo alishitakiwa na serikali kuwa ni mwongo!"

Kwa hiyo mwanzilishi wa Mashahidi ni Mwasherati, Mwongo na Mwizi! Sasa leo watu wanmwaminije huyo mwongo? Je! Musa alikuwa kama huyo au Yesu aliishi kama huyo? Hapana. Tuaamini Yesu kwa sababu alikuwa mwenye haki. Lakini Charles Russell? Hata siku moja.

Rutherford anajulikana sana kama nabii wa mwongo. Rutherford aliandika katika maisha yake kwamba,

"**watu Mamilioni wanoishi sasa hawatakufa.**" Alikuwa na mana kwamba Yesu atarudi karabuni. Lakini Rutherford alikufa katika mwaka wa 1942 na Yesu bado hajafika.

Tena Rutherford alifundisha kwamba Yesu atarudi katiaka mwaka wa 1914 na atapiga vita kuu. Lakini leo ni mwaka wa 2000, sasa tuwaulize Mashahidi, "Yesu yupo wapi?"

Kwa hiyo waanzilishi wao wawili walikuwa waongo sana. Sasa Shetani pia alikuwa mwongo sana katika bustani ya Edeni na ndiyo maana hatu wezi kuamini Shetani leo. Sasa kwa nini tuamini wale watu?

## Mafundisho Yao:

Kwanza wanafundisha waheshimu vitabu vyao zaidi ya Biblia. Katika gazeti lao "Watch Tower" toleo la 15/9/1910 ukarasa wa 298 walisifa maandishi yao yanayoitwa "Scripture Studies". Na kusema kwamba hakuna uwezo kwa watu kuelewa mpango wa Mungu kwa kusoma Biblia tu. Wanadai ukisoma Biblia pamoja na Scripture Studies basi unawezakuokoka. Lakini wanadai ukisoma Scripture Studies, kwa miaka kumi halafu ukaiachana kusoma Biblia kwa miaka miwili. Wanasema (katika ukurasa 298 katika toleo la juu) baada ya miaka miwili utarudi kwenye giza!

## Biblia Yasemaje?

1. Yn. 16:13, Yesu aliahidi msaidizi atakuja kwa mitume. Na Yesu alisema msaidizi ataongoza mitume katika nini? ____________________

2. 2 Tim. 3:15, Timotheo alipata wokovu kupitia nini? ___________________

3. 2 Tim. 3:16-17, Pumzi ya Mungu (Maandiko) yanafaa kwa ajili ya nini? _____________________________ _________________________________________________________________________________________.

4. 2 Pet. 1:3, Kupitia uwezo wa Uungu tulipewa nini ipasavyo kwa uzima? ______________________________

5. Ebr. 1:1-3, Mungu anaongea nasi leo kupitia nani? ____________________________
   Je, Kupitia Watch Tower? __________________

6. Sasa Mashahidi kama Katoliki wanadai hatuwezi kuelewa maandiko bila Watch Tower (Katoliki wanasema hatuwezi kuelewa maandiko bila Papa) lakini Yesu alisemaje katika Mt. 11:25? Mungu alifufanua nini? ___________________.

7. Yn. 8:32, Yesu alisema mtaifahamu kweli nayo hiyo kweli itawaweka? _________________

8. Yn. 17:17, kweli ni nini? __________________

## Hitimisho:

Dhehebu ya Mashahidi ya Yehova ni dini iliyoanzishwa na wanadamu. Na wale wanadamu hatuwezi kuwamini leo. Tusome Kumb. 18:18-22, tunahitaji kuagopa wale watu, kwa sababu wanatabiri vitu ambavyo havijatimizwa. Sasa alitabiri Yesu atakuja mwaka wa 1914, lakini wapi? Rutherford alisema, "Mamilioni ya watu wanpoishi sasa hawatakufa." Lakini yeye na wale wote wamekwisha kufa zamani. Rutherford mwenyewe alikufa mwaka wa 1942. Tena Rutherford anadai ukisoma Pumzi ya Mungu kwa miaka miwili

utarudi kwenye giza!   Lakini Biblia inasema wapi kwamba Pumzi ya Mungu haifai?   Ni lazima tuogope wale. Naamini kabisa Mungu anachukia sana wakati watu wanadai Pumzi yake haifai kupeleka mtu mbinguni!!! Tena Russell alikuwa mwasherati, mwongo na mwizi.   Na alijulikana sana kwa matendo maovu aliyofanya siku zile.   Juma lijalo tutamaliza somo kuhusu Mashahidi.

## Somo La Ishirini Na Moja                    Jina _______________

## Mafundisho Ya Madhehebu

**(Sehemu ya Nne)**

Kama tulivyoona juma lililopita kwamba Dhehebu la Mashahidi limeanzishwa na mwanadamu na tena wanakataa mamlaka ya Biblia na kuabudu Chama chao na mafundisho ya chama zaidi ya maandiko.   Leo tutaendelea na kuangalia badhi ya mafundisho yao.

**Mafundisho Yao:**
Chama Cha Watchtower wanafundisha Yesu sio Mungu bali ni malaika aliyeumbwa na Mungu.   Pia wanadai Yesu hakufufuliwa na mwili wake na wanadai Yesu ni Mikaeli, mmoja wa hao wakuu wenye cheo, Dan. 10:13.

**Mafundisho ya Biblia:**
I.   Tunaona Biblia hajawahi kusema Yesu ni Mikaeli au sawa na Mikaeli.   Maandiko yanataja Mikaeli mara tano
tu katika maandiko na hakuna hata sehemu moja inayoeleza kuwa Yesu ni Mikaeli.
- A. Dan. 10:13, inaeleza Mikaeli ni moja wa hao wakuu wa mbele.
- B. Dan. 10:21, inaeleza Mikaeli ni mkuu wa wana wa Israeli.
- C. Dan. 12:2, Jemadari mkuu, asimamaye upande wa wana wa watu wako (wana wa Israeli).
- D. Yuda 9, alishindana na Shetani.
- E. Ufu. 12:7, Mikaeli na malaika zake wakapigana na yule joka, Ufu. 12:7.
- F. Sasa ni mstari upi kati ya hii unaosema Yesu na Mikaeli ni mtu moja?

II. Thibitisho zaidi inaonyesha Yesu sio Malaika.
- A. Yoh. 5:23, tunaona tunatakiwa kumheshimu Yesu kama tunavyoheshimu Baba.
- B. Ebr. 1:6, Baba ameamuru malaika wote wamwabudu Yesu.
- C. Yoh. 1:1-3, 7, 14, mwanzoni Yesu alikuwa na Mungu na alikuwa Mungu.
- D. Yoh. 8:58;   Ufu. 1:8; 21:6;   22:13, Yesu hakuumbwa na Baba bali alikuwa muumbaji

III. Maandiko yanaonyesha Yesu ni mtu moja na amefufuka.
- A. Yoh. 2:19-22, Yesu alisema ata________________?
- B. Yn. 20:24-28, Yesu alionyesha nini kwa Tomaso?   _____________________
- C. Zab. 16:10, Daudi alitabiri nini? ___________________________________
- D. Mdo. 2:30-31, Petro alidai nini kuhusu Yesu? ________________________
- E. Mdo. 1:1-3, Yesu alikuwa hai au ni mtu mwingine hapa?   _______________
- F. Mdo. 1:11;   Efe. 4:10;   Ebr. 10:12, ni yule yule aliyefufuka au mtu mwingine?   _______________

IV. Tujue maandiko yanafundisha kuwa Yesu na Baba ni kitu kimoja.
- A. Yoh. 1:1-3, 7, 14, Neno alikuwa _______________?
- B. Yoh. 17:5, Yesu alikuwa __________________?
- C. Flp. 2:6, Yesu ni sawa na ____________________?
- D. Pia soma Yn. 14:11 na 17:21.

**Hitimisho:**

Tumeona kwa majuma mawili ya kuwa Dhehebu la Mashidi Wa Yehova wanafundisha na wanaamini tofauti sana na Biblia. Kwanza wanaheshimu vitabu vyao zaidi ya Biblia. Tena wanakataa Uungu wa Yesu Kristo. Kama Kanisa la Kristo leo tunavyoamini sana Maandiko na Yesu ni Mungu aliyekufa na aliyefufuka kwa ajili ya kila mtu. Kama watu wanapinga Biblia na Yesu ambaye anamamalaka yote hapa ulimwenguni, Mat. 28:18-20, tuachane nao.

## Somo La Ishirini Na Mbili                    Jina _______________

## Je, Kuna Lo Lote Katika Jina?

Kama utaangalia ulimwengu wa dini leo utaona majina mamia yanatumika na watu kwa kutambua dhehebu au mafundisho yao. Lakini tukiangalia mara moja tu katika maandiko tutaona majina mengi tunayosikia leo hayapo kwenye kitabu cha Mungu. Kwa maana watu wengi wanajiita majina ambayo hayaonyeshi heshima kwa Yesu na Baba yake.

### I. Kwa nini ni vibaya kutumia majina yamelaumiwa na wanadamu?

A. Kwanza majina ya wanadamu limehukumiwa katika Agano Jipya.
1. 1 Kor. 1:10, Paulo alitufundisha kuwa tunena mamoja, tusiwe na ___________, na tujiunge pamoja katika ____________ ___________ na hukumu _______________.
2. 1 Kor. 12-13, Paulo alihukumiwa watu ambao walitumia majina tofauti.
3. Tena aliuliza, Je, Kristo _____________?
4. Je, Paulo ___________ kwa ninyi? Ulibatizwa katika jina la ___________?
5. Paulo alikuwa ana kataa kabisa watu wasijiite kwa majina ya wanadamu. Hata jina lake alikataa watu wasitumie.
6. Tunahitaji kuweka heshima wetu kwa wale wanastahili heshima. Na hakuna hata mtu moja alikufa kwa ajili yetu na hatuwezi kubatizwa katika jina la mtu yo yote ila Yesu Kristo, Rum. 6:1-4.
7. Kwa hiyo kama tunajiita kwa jina la mtu mwingine basi tunaheshimu huyu zaidi ya Yesu. Kwa Mfano Luther, watu wengi sana siku hizi wanajiita Waluteri, Je? Martin Luther alisulubiwa kwa ajili yao? Tumesikia Paulo hapa kwa makini.

### II. Majina ya maandiko kwa ajili ya Kanisa.

A. 1 Kor. 1:2, Kanisa la _______________.
B. Ebr. 12:23, Kanisa La __________________________________.
C. Rum. 16:16, Makanisa ya ____________________.
D. Kol. 1:24, Mwili wa _________________________.
E. Ufu. 21:2, ___________________ ya Kristo.
F. 1 Tim. 3:15, Nyumba ya _____________________.
G. Tazama hapa, majina yale sio ya dhehebu. Na haelezi kanisa tofauti, majina yale ya juu yanaeleza Kanisa la Kristo, Kanisa la Mungu la peke. Katika kila jina hapa juu tunaona Yesu na Baba wanatukuzwa. Na kwa sababu majina yale yanapatikana katika maandiko basi majina yale yametokea kwa Baba.

### III. Lakini jina zuri halitoshi.

A. Ni lazima tufuate taratibu tunaopata katika Agano Jipya, 2 Yoh. 9-10.
B. Kama kuna kundi la watu na wanatumia jina zuri bado wanahitaji kufuata maandiko kama yalivyoandikwa. Bado watahitaji kuishi, kuabudu, kufanya kazi kama kusudi la Mungu.
C. Kuna madhehebu mengi wanatumia jina zuri lakini mafundisho yao ni mabovu. Mungu haiwezi kufurahisha na watu wale, Gal. 1:6-9.
D. Kwa sababu ni lazima _____________________, 1 Thes. 5:21.
E. Ni lazima tufuate mamlaka ya Yesu (Mat. 28:18-20) kwa sababu yeye amewekwa kuwa juu ya vitu vyote, Efe. 5:23-24 na Kol. 1:18.

### IV. Jina La Mkristo.

A. Makanisa la Kristo wanajiita kila mtu kuwa “Mkristo”. Na kila Mkristo anafanya Kanisa la Kristo.
B. Katika maandiko watu wa Kanisa la Kristo wanajulikana kuwa Wakristo, Watakatifu, Watoto, Wanafunzi, Makuhani na ndugu. Jina Mkristo inaeleza na inaonyesha sisi ni mali ya Kristo, Mdo. 11:26. Vile vile jina lako kamili inaonyesha wewe ni mtoto wa Baba yako.
C. Tunajiita Wakristo kwa sababu ya Mdo. 11:26.
D. Kila Mkristo ni Mtakatifu kwa sababu dhambi zenu zimesafishwa, Rum. 1:7.
E. Kila Mkristo ni Mtoto wa Mungu kwa sababu tumezaliwa tena, 1 Pet. 1:22-23.
F. Kila Mristo ni Mwanafunzi kwa sababu tunajifunza kuhusu Yesu, Yn. 15:8.
G. Kila Mkristo ni Mkuhani kwa sababu tunaabudu na tunatumikia Mungu kupitia Yesu, 1 Pet. 2:5.
H. Kila Mkristo ni ndugu kwa wote ambao wana Baba moja, Ga. 6:1.
I. Kwa watu wanaopenda na wanaoheshimu Yesu na Baba yake tutajiita na tutajulikana mbele ya watu kwa kutumia jina la Mungu au Yesu. Na tutatumia majina yale kwa sababu Mungu ameyaamuru. Na tutakataa majina ya wanadamu kwa sababu sisi sio watoto wa mwanadamu yo yote bali ni watoto wa Mungu.

## V. Sasa kuna nini katika jina?

A. Kuna watu wengi wanafikiri kwamba hakuna kitu muhimu katika jina, lakini mimi sikubaliana nao kwa sababu ya Mdo. 4:12.
B. Kuna jina juu zaidi ya majina yote, na jina lilo ni Yesu.
C. Hakuna jina lingeni lina nguvu na mamlaka kama jina la Yesu Kristo.
D. Na kama Mungu ameona ni vyema tutumia jina la Kristo sisi ni nani kubadirisha mawazo ya Baba?

## VI. Kwa nini tutumie jina tulilopewa na Mungu?

A. Kupitia jina lake tu tunaweza kuokolewa, Mdo. 4:12.
B. Kwa jina lake kila mtu atapiga _______________, Flp. 4:11-12.
C. Sisi tuliyobatizwa tuko kwenye nyumba ya Baba, kwa hiyo tujulikana kwa jina la Baba, 1 Tim. 3:15; Efe. 3:14-15.

## Hitimisho:

Kupitia maandiko tunaweza kuona ni lazima tujiite na tutumia jina lililotolewa na Mungu. Bila kujali tunasikia au tunaamini nini ni lazima tufuate maandiko (Rum. 10:17). Njia au jina lo lote haifai (Mith. 14:12). Katika maneno ya Mungu tu tunaweza kupata njia iliyosahihi, Zab. 119. Ni lazima tutumia majina yaliyotolewa na Mungu, ilikuonyesha tunamheshimu yeye. Na ni lazima tumpendeze yeye kama tunataka yeye atupokee sisi siku ya mwisho, Yn. 14:2-3.

**Somo La Ishirini Na Tatu** **Jina _______________**

## Maandiko Yanasema Nini Kuhusu Uungu?

Makanisa ya Kristo wanawajibu wa kufundisha ukweli kuhusu yote. Tukishindwa kufundishwa ukweli tunaelewa tutapotea, Mat. 7:21. Kwa hiyo ni wajibu wetu na mapenzi yetu kufundisha yote yaliyotoka juu kwa Baba. Na fundisho moja kati ya mengi ni fundisho kuhusu Uungu.

### I. Tufafanue Uungu.

A. Neno "Uungu" limetumika mara mbili katika Biblia ya Ki-Swahili na mara tatu katika Biblia ya Ki-Ingereza (Ki-Swahili na Ki-Ingereza-Mdo. 17:29; Rum. 1:20; Ki-Ingereza Kol. 2:9). Kufuatana na kamusi ya Ki-Yunani kila mstari unatumia neno tofauti lakini maana ni sawa.

B. Lakini ni muhimu kwa sisi tuelewa neno "Uungu" ni nafsi tatu zinafanya Mungu. Lakini wakati tunafikiri kuhusu neno "Uungu" tusifikiri kwamba kuna watu watatu. Kwa sababu ni moja tu kati ya nafsi tatu zilifika hapa ulimwenguni.

1. Yesu ambayo ni neno alivaa _______________, Yon. 1:1, 7, 14.
2. Ni Yesu tu anajulikana kuwa mwanadamu, 1 Tim. 2:5.
3. Aliacha hali yake ya Uungu ili aje kama mwanadamu, Flp. 2:6-7.
4. Yeye tu alikufa na alimwaga damu kwa ajili ya wote, Flp. 2:8-11.
5. Na yeye tu alikuwa mtu na Mungu.
6. Soma 1 Tim. 3:16.

### II. Nafsi tatu lakini Mungu moja.

A. Watu wengi siku hizi wanashindwa kuelewa jinsi Mungu alivyo. Ni kwa sababu katika hali ya mtu sisi hatuna ufahamu kama Mungu kwa hiyo kuelewa mambo ya Mungu ni vigumu. Lakini kama hatuelewi kidogo jinsi Mungu alivyo basi ni kosa la letu kwa sababu amefafanua wenyewe katika maandiko, Efe. 3:4.

B. Biblia inatufundisha kuna Mungu moja, Efe. 4:6.

1. 1 Kor. 8:6, Kwetu kuna _________________.
2. Zek. 14:9, Bwana ____________ na Jina _______________.
3. Isa. 42:8, Mungu ndiyo ______________.

C. Sasa tunatambua kuna nafsi tatu kati ya Mungu, Mat. 28:19.

1. Nafsi tatu ni ________________, ________________________ na _________________________.

D. Pia tunahitaji kuelewa neno "Mungu" pia ina maana "Uungu" au "Umungu".

1. Na Baba, Mwana na Roho Mtakatifu wanashirikiana katika hali ambayo tunafahamu ni Mungu.
2. Wayahudi walishindwa kuelewa haya, Yn. 10:30-31; Yn. 8:58.
   a. Kwa sababu walitaka kumuuwa Yesu alipodai yeye na Baba yake ni kitu kimoja.
   b. Yn. 10:32-33.
   c. Walishindwa kuelewa Uungu anaweza kuchukuwa hali ya mtu wakati bado ana hali ya Mungu kule mbinguni.

### III. Baba Na Mwana.

A. Maandiko yanaeleza sana na yanaonyesha Baba na Mwana ni nafsi mbili tofauti.

1. Hata Yesu aliposema "Baba na Mimi ni moja", Yn. 10:30, Mimi =1 na Baba =1 (1+1=2). Tunaona hapa nafsi mbili.

B. Lugha ya Biblia inaongea kuhusu nafsi mbili.

1. Mungu aliye Baba sio mwanadamu bali ni Uungu.
2. Mungu aliye Yesu alikuwa Mungu na akavaa mwili kwa muda na akarudi mbinguni, Ebr. 10:5.

C. Injili ya Yohana ni kitabu kizuri kinaeleza Uungu.

1. Yn. 3:16, Tuna mtoaji na yule ambaye ni zawadi. Kwa hiyo walikuwepo wawili.
2. Yn. 3:13, Yeye aliyepanda mbinguni ni yule aliyeshushwa kutoka mbinguni, moja alikuwepo hapa ulimwenguni wakati moja alikuwepo mbinguni.
3. Yn. 6:44-45, Moja hawezi kwenda kwa Baba asipokwenda kwa nani kwanza? _______________
4. Yn. 7:33, Yesu alikuwa aenda kwa nani? Nani alimtuma yeye? Kwa maana walikuwepo wawili!
5. Yn. 8:16, Yesu hayupo peke yake bali upo na atahukumu na ________________.
6. Yn. 8:17-18, tunaona tena kuna nafsi mbili ambazo ni washahidi.
7. Na kuna mistari mingi inayoleza kuwa kuna nafsi mbili, Baba na Mwana. Na wale wawili ni wamoja. Yn. 8:28, 42; 10:36; 12:27-30, 44, 49; 14:10, 15-17, 23-24, 26, 28.
8. Mwishoni katika Yn. 16:7-13, tunaona nafsi tatu. Tunaona Baba (nafsi moja) Yesu (nafsi ya pili) na Roho Mtakatifu (nafsi ya Tatu). Kwa hiyo nafsi tatu lakini Mungu moja, Uungu.

## Hitimisho:

Biblia inatufundisha kwamba Mungu ni nafsi tatu, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Kila mmoja ni nafsi tofauti. Baba sio Roho, Roho sio Yesu na Yesu sio Baba. Lakini wote wanashiriki katika Uungu au Mungu. Wote wanafanya kazi pamoja, wana nia moja, na wanaitwa Mungu.

**Somo La Ishirini Na Nne** **Jina_______________**

## Kuna Vitu Vingapi Kwenye Maandiko Ni Vya Milele?

Kuna mafundisho mengi siku hizi kuhusu kila aina ya mafundisho. Na kuna watu wengi wanafundisha kinyume na maandiko kwa sababu hawajui maandiko au hawajali ukweli. Lakini bila kujali watu wa leo wanafundisha nini, sisi leo tutaangalia vitu vya milele. Kwa sababu kuna watu wanafundisha leo kwamba Ufalme wa Yesu sio ya milele. Wapo watu wengine wanafundisha jehanum sio ya milele, lakini tuangalie Maandiko.

### I. Mungu ni wa Milele.

A. Isa. 41:4, Mungu ni ________________ na _______________.
B. Ufu. 1:8, Mungu ni ________________ na ________________.
C. Rum. 16:26, Mungu ni wa __________________.

### II. Roho Mtakatifu ni wa Milele.

A. Ebr. 9:14, Yesu alijitoa mwenyewe kupitia Roho wa __________________.

### III. Ukombozi ni wa Milele.

A. Rum. 3:24, 25, Tunahesabiwa haki kupitia njia ya _______________.
B. Efe. 1:7, Kupitia damu yake tunao _________________.
C. Ebr. 9:12, Aliingia mara moja tu mahali Patakatifu, akapata kwa ajili yetu ukombozi wa ________________.

### IV. Wokovu ni wa Milele.

A. Mdo., 4:12, Kuna wokovu katika jina la _________________.
B. Ebr. 9:28, Mungu anatalajia sisi wote tutafute na kupata ________________.
C. Ebr. 5:9, Yesu ni mwandishi wa ____________ kwa ________________.

### V. Ufalme wa Mbinguni ni wa Milele.

A. Mat. 6:33, Tunatakiwa kutafuta kwanza _____________________.
B. Yn. 3:1-8, Tusipo _______________ tena hatuwezi kuona ___________________.
C. Rum. 14:17, Hali ya ufalme wa Mungu ni wa ____________________.
D. 2 Pet. 1:11, Ufalme ni wa ____________________.

### VI. Ufalme wa Shetani ni wa Milele (Jehanum).

A. Marko 9:43, Moto wa jehanum __________________.
B. Mat. 18:8, Watatupwa kwenye moto wa _______________________.
C. Mat. 25:46, Na waliopotea wataingia katika _________________________________.
D. Mat. 25:41, Waliolaniwa wataingia kwenye _______________________.

### Hitimisho:

Kwa kweli kuna vitu vingi ni vya milele. Kuna vingine hatujagusa leo. Lakini kwa watu wale ambao wanafundisha Mungu, Mbinguni au Jehanum sio ya milele basi wanapinga mafundisho ya Biblia. Ukweli ni Mungu ni wa Milele, Ufalme wake ni wa Milele na kwa hao watashindwa kuingia katika Ufalme wa Mungu basi watatupwa kwenye Ufalme wa Shetani kwa milele.

## Somo La Ishirini Na Tano

**Jina ______________**

## Je, Sisi Ni Makuhani Wa Mungu?

Mimi ni kuhani. Wewe ni kuhani kama umezaliwa tena katika ufalme wa Mungu. Kwa hiyo kama tumezaliwa tena basi sisi wote ni makuhani katika ufalme wa Mungu na Yesu Kristo ndiye Kuhani Mkuu. Kwa hiyo Biblia inatufundisha wazi kwamba wakristo wote ni makuhani. Lakini baada ya kufunguliwa ufalme wa Mungu watu walianza kufundisha kwamba kuna wakubwa tu ambayo ni makuhani. Ndiyo maana leo katika madhehebu mbali mbali wanao Makuhani na washiriki tu wa kawaida. Na wanamini ndiyo kazi tu ya Mkuhani kutoa "Sakramenti" kwa Mungu. Lakini tutaangalia leo, Makuhani ni nani na Kazi yao ni nini?

### Kuhani ni Nini?

Neno "Kuhani" katika Agano Jipya lina maana mtoto wa mfalme au mtumishi. Na makuhani wote kwenye maandiko ni lazima wawe na madhabahu na ni lazima watoe sadaka. Na hakuna mtu kwenye maandiko alikuwa na uwezo wa kutoa sadaka kwa ajili ya watu mbele ya Mungu. Ndiyo Manabii wengi wametoa sadaka, lakini kazi ya manabii ni kutumikia Mungu kwa ajili ya watu. Lakini kazi ya Kuhani ni kutumikia Watu mbele ya Mungu. Kwa tofauti ipo. Na hata leo kama wewe ni kuhani ni lazima utoe matoleo na sadaka kwa Mungu.

### Kuhani Wetu Leo Kama Kanisa.

Hatuwezi kusoma kuhusu Ukuhani wa Yesu mpaka kitabu cha Waebrania katika Agano Jipya. Na hapa mwandishi anamtukuza yeye kama Kuhani Mkuu wa pekee na wa milele. Yeye tu ni Kuhani Mkuu wetu na hakuna mwingine. Amekwisha mwaga damu yake kwa ajili yetu na damu yake yanafaa milele. Lakini Ukuhani wetu umetajwa kidogo sana katika kitabu cha Waebrania. Ni Ebr. 10:22 inafundisha sisi jinsi tunavyokuwa Makuhani. Na Ebr. 13:15-16, intufundisha tunahitaji kutoa matoleo gani kwa Mungu.

### Waebrania 13:15-16.

Hapa tunaona mwandishi wa kitabu hiki anaongea kuhusu kazi ya Mkristo ambaye ni kazi ya kuhani tena. Kwa hiyo tunaona hapa kwamba sio Makuhani walionahaki ya kutoa sadaka kwa Mungu. Sio sadaka ya Wanyama bali sadaka Mungu anayohitaji siku hizi.

### 1 Pet. 2:5-9.

Petro katika barua hii anaongea na Wakristo waliotawnyika sana. Na katika mstari wa tano Petro anasema ninyi nanyi? ______________________ na _________________________. Alikuwa ana onyesha Wakristo wa leo wanayotakiwa kuachana na dunia na kwa hiyo Wakristo sio Hekalu tu (1 Kor. 6:16-20) bali ni makuhani katika miili yao. Tena katika mstari wa tisa aliongeza kwamba sisi ni "Ukuhani wa kifalme". Alikuwa na tukuzwa hali yetu ya kiroho na uhusiano wetu na Mungu. Na leo kwa sababu sisi ni Makuhani basi ni lazima tutoa matoleo au sadaka kama Mungu anavyotaka leo na ni laimza tukumbuke kuwa ni Makuhani tu walioamriwa kutoa sadaka. Na kama Makuhani au watu wa Mungu sisi ni mali yake, na kama tu mali yake tunakaribia kiti cha ufalme wake kupitia Kuhani Mkuu Yesu Kristo, 1 Tim. 2:5.

### Ufunuo 1:6.

Yohana mtume aliyependwa sana na Yesu anakumbusha sisi katika mstari huu kwamba Kristo alitufanya sisi, "Kuwa ufalme, na makuhani kwa Mungu." Kwa jumla sisi wote ni Ufalme wake lakini peke yetu kila moja ni kuhani katika Ufalme wake. Ndiyo, Yohana mwenyewe alitufundisha sisi kuwa ni makuhani mbele za Mungu. Hakusema walikuwa wachache ndani ya Kanisa ambao ni Makuhani lakini ni sisi wote, tena alirudia maneno yale yale katika 5:10.

### Warumi 12:1.

Angalia maneno machache hapa: "Ndugu...Dhabihu....Ndiyo ibada yenu yenye maana." Ndugu sio watu waliochagulia na kusoma shule fulani walikuwa na kutoa dhabihu au ibada yenye maana. Ni Wakristo wote! Kwa sababu tunajua Makuhani tu wanaweza kutoa sadaka katika Agano Jipya, mstari huu unaonyesha ndugu ni makuhani na ni lazima tutii mstari huu. Kwa hiyo ni lazima tushukuru tu kwamba sisi wote ni makuhani na hatuhitaji kupitia mtu au mwanadamu ye yote ilitufike kwa Mungu. Ni kupitia Yesu tu.

## Matoleo au Sadaka ya Kuhani ni Nini Leo?

Tumesoma sehemu nyingi, tayari tumeona kazi nyingi ya kuhani siku hizi chini ya Agano Jipya. Kwa hiyo tuangalie oradha ya kazi tunayoweza kufanya kazi zile ni kama sadaka kwa Mungu.

**Imani yetu ni Sadaka.**
**Upendo wa Mungu si Sadaka wetu.**
**Kutubu kwetu ni Sadaka.**
**Kukiri imani katika Yesu Kristo ni Sadaka.**
**Kubatizwa katika Kristo ni Sadaka.**
**Kumsifu Mungu ni Sadaka.**
**Kutoa ni Sadaka.**
**Kuimba ni kutoa Sadaka.**
**Kuomba ni kutoa Sadaka.**
**Maisha ya kumshima Mungu na kumpenda ni sehemu ya maisha yetu na tena ni Sadaka.**

## Hitimisho:

Kwa matoleo ya juu Mungu anashukuru sana kama tunatoa kupitia Yesu Kristo Bwana wetu. Kwa hiyo tunaweza kutoa sadaka kwa sababu sisi ni Makuhani wa Mungu.

## Somo La Ishirini Na Sita                                        Jina _______________

## Ulevi.

Kwa kweli leo ulimwengu umechanganya watu. Mpaka watu wanafikiri wanaweza kutembea kama Yesu na kulewa kila mara. Ni wapi kwenye maandiko unaona Yesu alilewa? Ni wapi kwenye maandiko unaona Yesu alikuwa na haribu mwili wake na kileo? Ni wapi kwenye maandiko unaona Yesu alikwenda kilabuni iliashirikiane na ulimwengu? Gal. 5:19-21 inaonyesha kwa ufupi walevi wote sehemu yao ni kwenye moto wa milele.

I. Ulevi Ni Dhambi.

A. Hos. 4:11, Divai huondoa ______________.
B. Efe. 5:18, Msilewe kwa mvinyo ________________.
C. Gal. 5:19-21, ni tendo la _______________.
D. 1 Pet. 4:3, Ni mapenzi ya _______________ wasiomjua ________________.
E. 1 Kor. 6:1, Walevi hawataiingia katika ______________________.

II. Matokeo Ya Ulevi Ni:

A. Mit. 21:17; 23:21, ___________________.
B. Mit. 23:29-30, __________________.
C. Isa. 28:7, __________________.
D. Isa. 28:8, ________________________.
E. Mit. 20:1, _________________________.
F. Isa. 5:11-12, _______________________.
G. Luka 21:34, ________________________.

III. Mifano Ya Ulevi:

A. Mwa. 9:21, Alipata taabu gani? ______________________.
B. Mwa. 19:31-35, Lutu alilala na _____________________.
C. 1 Sam. 25:36, ______________________.
D. 1 Kor. 11:21, Paulo alimwambia Wakorintho nini? ______________________________.

IV. Adhabu Ya Walevi:

A. Hab. 2:15, ______________________.
B. Mit. 23:31-32, ________________________.
C. 1 Kor. 5:11, ______________________________.
D. 1 Kor. 6:10; Gal. 5:11, ___________________________.
E. Mat. 24:48-51, _______________________________________.

Hitimisho:

Biblia haizungumzi kuhusu vileo, ulevi kama ni kitendo kizuri. Bali tunaona ni wajinga tu wanaweza kuharibu maisha yao ya hapa ulimwenguni na kupotea milele kwa sababu ya vileo. Tutembea kama Yesu, tuwe watakatifu na kutafuta mambo yaliyojuu siyo ya ulimwengu huu.

## Somo La Ishirini Na Saba                    Jina _______________

## Ndoa

Tukisoma mwanzo wa uumbaji katika Mwanzo 1-3, tunaona Mungu aliumba mwanamke moja kwa ajili ya mwanaume. Ni mpango wa Mungu kila mwanaume awe na msaidizi wake na msaidizi wake awe mwanamke. Mungu hakuumba wanawake wawili au zaidi kwa Adamu bali moja tu na ndivyo inavyotaka leo. Bila kujali tunataka nini, Mungu aliumba mwanamke kwa mwanaume, siyo wanawake kwa mwanaume!

### I. Ndoa Ilianzishwa Na Mungu:

A. Mwa. 2:18, Mungu hakutaka mwanaume aishi peke _________________.
B. Mwa. 2:18-22, Mungu aliumba mwanamke awe ____________________.
C. Mwa. 2:23-24; Mat. 19:5-6, ndoa ya kwanza ilianzishwa na _____________________.
D. Malaki 2:14, ____________ ni shahidi wa _________________.
E. Ebr. 13:4, Ndoa iheshimiwe na ______________.
F. 1 Kor. 7:1-5, Ni njia ya kuzuia zinaa.
G. 1 Kor. 7:7-9, Ni njia ya kuzuia tamaa mbaya.
H. Mat. 19:6, ____________________ na Mungu, mwanadamu ___________________.

### II. Dhambi Katika Ndoa:

A. Kuwa na wanawake zaidi ya mke moja:
1. Mwa. 1:27, 28; 2:22-23, Hapo mwanzo Mungu alimpa Adamu mke _____________.
2. Mwa. 2:24; Mat. 19:4-5, Na mwanaume pamoja na mwanamke wakawa __________________.
3. Mwa. 4:19, Kuoa wanawake wengi kulianzishwa na ukoo mbovu wa _________________.
4. Ingawaje baadhi ya wanaume wa Agano La Kale walikuwa na wake wengi, walipata tabu sana kwa kufanya hivyo:
   a. Ibrahimu - Mwa. 16:4-6; 21:9-10.
   b. Daudi - 2 Sam. 13:1-38; 2 Sam. 15:18.
   c. Sulemani - 1 Fal. 11:1-8.

   Taja matatizo walikuwa nayo Ibrahimu, Daudi na Sulemani kwa sababu walioa wengi.

   ______________________________________________________________________________

   ______________________________________________________________________________.

5. Yesu Kristo alikataa tabia hii ya kuoa wake wengi, Mat. 19:4-5.
6. Roho Mtakatifu alifundisha kwamba kila mwanaume anapaswa kuwa na mke, 1 Kor. 7:1-3.
7. Mtu yeyote atakayeoa au kuolewa na mwingine anazini, Rum. 7:2-3; Gal. 5:19-21.

B. Kutengana Au Talaka:

1. Tunaweza kuoa au kuolewa kwa watu gani?
   a. 1 Kor. 7:9, ______________________.
   b. Wale ambao walio au waliolewa lakini mwezako akifariki, Rum. 7:2-3.
   c. Wale walioachana na mwenzake kwa sababu ya uasherati, Mt. 19:9 (Lakini hatuna uwezo kuoa au

kuolewa kwa yule alioachwa kwa sababu ya uasherati).

Hitimisho:

Tukumbuke ndoa ilianzishwa na Mungu, na ni lazima tufuate maneno yake kama tunataka Mungu atubarikie ndoa zetu. Na kama Mungu atakataa kubariki ndoa zetu kwa sababu ya uasherati au mitala ni lazima tuache dhambi kama tunataka kurithi ufalme wa mbinguni.

## Somo La Ishirini Na Nane — Jina _______________

## Kanisa La Kristo Sio Dhehebu

(Sehemu ya Kwanza)

Fedha tunazotumia zimegawanyika katika aina tofauti, 10,000/-, 5,000/-. Na taratibu za siasa zimegawanyika, CCM, TLP. Kwa hiyo tunaona kupitia mifano kwamba neno "dhehebu" ni magawanyiko au kundi fulani. Katika ulimwengu wa dini, "Dhehebu" ni jamii ya watu waliotengana na Kanisa lilianzishwa na Kristo. Ndiyo katika Agano Jipya Biblia inazugumza kuhusu makusanyiko (1 Kor. 1:2) au Kanisa zima (Efe. 1:22-23). Lakini wale watu kwenye makusanyiko walikuwa Wakristo katika Kanisa la Kristo. Hawakuwa Walutheri katika Kanisa la Moravian.

### I. Kanisa La Kristo Ndilo Kanisa la Karne ya Kwanza.

A. Tuangalie yaliyo kweli.
- 1. Kanisa la Kristo siyo Kanisa la Wayahudi.
  - a. Agano la Kale, msingi wa Wayahudi ulitolewa, Rum. 7:1-4; Kol. 2:14-17; Ebr. 8:8-13.
- 2. Kanisa la Kristo siyo "Protestant" kundi la watu waliochukia na mafundisho ya Katoliki kwa hiyo wakaacha kusali na wakaanzishwa makanisa yao.
  - a. Madhehebu yote yalianzishwa baada ya karne ya kwanza na kama kuna kundi la watu walianzisha bada ya karne la kwanza na wanadamu, basi hawa watu hawawezi kuwa Kanisa lililojengwa na Kristo.
  - b. Kanisa la Bwana wetu alilianzisha katika karne ya kwanza mwaka wa 33, Marko. 9:1; Mdo. 1:8; Mdo. 2:1-4, 47.
- 3. Vitendo vya madhehebu havimo katika Kanisa.
  - a. Madhabahu ya maombi.
  - b. Kupiga kura kwa watu wanaotaka kujiunga.
  - c. Vyombo vya muziki.
- 4. Kanisa la Kristo sio Kanisa la Katoliki.
  - a. Kanisa la Katoliki lilianzishwa katika mwaka wa 606 Bk, karibu na miaka 600 baada ya maisha ya Yesu.
  - b. Na tukiangalia mafundisho ya Wakatoliki tutaona kwa ufupi hawapati mamlaka yao kutoka kwa Mungu.

### II. Fafanuzi ya Kanisa.

A. Neno "Kanisa" limetoka kwenye neno ya Kiyunani "Ecclesia," na maana yake ni "Walioitwa".
- 1. Kwa hiyo Kanisa ni mwili wa watu walioitwa kutoka ulimwenguni, 2 Thes. 2:14.
  - a. Kwa kutii injili, 2 Thes. 1:7-9.
- 2. Kanisa linaongozwa na Kristo, kichwa cha Kanisa lake, Kol. 1:18.
- 3. Na Roho anakaa ndani ya Kanisa, Efe. 2:22-23.

B. Kanisa ni moja katika hesabu.
- 1. Yn. 10:16, Kuna kundi ngapi? __________________
- 2. Na Kanisa ndiyo kundi lile, Mdo. 20:28.
- 3. Tena kuna mwili moja, Efe. 4:4.
- 4. Na mwili ni Kanisa, Efe. 1:22-23.
- 5. Tunajua Yesu alifundisha kuhusu ndoa tunaweza kuwa na mke moja tu, Mat. 19:1-9; Rum. 7:1-4.
- 6. Na Kanisa ni mke wa Yesu, Efe. 5:22-23.

**Hitimisho:**

Tutaendela kujifunza kuna Kanisa moja tu. Wazo la Kanisa moja naona tumeelewa. Lakini labda tumeelewa kwa maneno na siyo kwa matendo kwa sababu mara nyingi watu wanaanguka na wanajiunga na madhebu. Kwa maana hawakuelewa vizuri mafundisho ya Kristo ndiyo maana wanapotea.

## Somo La Ishirini Na Tisa    Jina _______________

## Kanisa la Kristo Sio Dhehebu

(Sehemu ya Pili)

Kanisa la Kristo ndilo lile la karne ya kwanza. Na tunaweza kuthibitisha hayo kupitia sifa za Kanisa la Awali na sifa tulizo nazo.

| Kanisa La Karne Ya Kwanza | Kanisa La Karne Ya Ishirini Na Moja |
|---|---|
| a) Majina ya Kanisa:<br>Kanisa la Kristo - Rum. 16:16<br>Kanisa la Mungu - 1 Kor. 1:2<br>Kanisa la Bwana - Mdo. 20:28. | a) Kanisa la Kristo la leo linatumia jina lile linalopatikana katika kitabu cha Warumi 16:16. Kwa hiyo tunatumia jina lile Wakristo wa karne ya kwanza walikuwa wakitumia jina hilo. |
| b) Madaraka:<br>Maaskofu, Washemasi, Wahubiri na Washiriki walikuwepo kwenye makusanyiko kama watu walikuwa na sifa za kazi, Fil. 1:1. | b) Leo taratibu ya viongozi kwenye Kanisa ni lile lile, hakuna mabadiriko. |
| c) Ibada:<br>Walikutana siku ya kwanza ya juma, 1 Kor. 16:2.<br>Waliimba sifa kwa kutumia midomo tu, Efe. 5:19.<br>Waliomba, walihubiri, walichukua meza ya Bwana na walitoa changizo, Mdo. 2:42, 47; 1 Kor. 14:15; 16:2; Mdo. 20:7. | c) Kanisa la Kristo leo linakutana kila siku ya kwanza ya juma. Katika ibada tunaiimba bila vyombo vya muziki, tunaomba, tunashiriki Meza ya Bwana na tuna toa kama karne ya kwanza. |
| d) Mwongozo:<br>Walifuata mafundisho ya mitume kwa mamlaka ya imani na matendo yao, Mdo. 2:42; Gal. 1:6-9; Ufu. 22:19. | d) Kanisa la Kristo leo linaongozwa na mafundisho ya mitume tu, hatuna mwongozo zaidi ya Agano Jipya. |
| e) Kama Ulitaka Kujiunga Nao:<br>Ni lazima uamini, utubu, umkiri Kristo na kubatizwa na maji mengi, Mdo. 8:26-40. | e) Vile vile leo hatuna tofauti hata kidogo, tuko sawa kabisa. |
| f) Huduma:<br>Kushika yaliyo kweli katika nyumba ya Mungu, 1 Tim. 3:15. | f) Kanisa la Kristo leo linashika maneno ya Yesu na Mungu kama ilivyo kweli yote, hatuongezi au hatupunguzi hata kidogo. |

**Hitimisho:**

Kitu kinachofanyika kwa ujumla, siyo kwa sehemu tu. Kwa hiyo unaweza kuona Kanisa la Kristo la leo si kwamba linafanana au likokaribu na Kanisa la Awali, bali Kanisa la Kristo la leo ni Kanisa la Awali, hakuna tofauti hata kidogo. Kwa hiyo kwa sababu tuko sawa basi sisi pia ni Kanisa la Kristo.

**Somo La Thelathini** **Jina _______________**

## Kanisa la Kristo Sio Dhehebu

(Sehemu ya Tatu)

1. Bwana wetu hakujiunga na chama au mugawanyiko wakati alikuwa ana tembea pamoja ulimwenguni. Wakati alikuwa ana ishi hapa ulimwenguni, madhehebu manne yalikuwepo ya Wayahudi; Farisayo, Sadukayo, Herodia na Esseni. Lakini madhehebu haya yalifundisha ukweli kidogo, Bwana wetu hakufuata hawa watu.

2. Tena tunafahamu Bwana wetu aliomba kwa umoja, Yh. 17:20-21. Tena Bwana wetu alinunua umoja, ambao ni kinyume na madhehebu, Efe. 2:16. Tena aliomba sana tusiwe na faraka bali tunena mamoja, 1 Kor. 1:10. Tena alipanga kwamba tutakuwa na umoja, Efe. 4:1-6. Kwa hiyo Bwana wetu hakuwa na dhehebu na alikuwa kinyume na madhehebu. Kwa hiyo Kanisa lake ni lazima tufuate mapendekezo yake.

## Tupime Kanisa Lililojengwa Na Yesu Na Madhehebu.

| Kanisa La Agano Jipya | Madhehebu |
| --- | --- |
| (1) Uungu ulianzishwa: Mat. 16:18; Dan. 2:44. | (1) Yanaanzishwa na Wanadamu, bila msaada wa Uungu. Mungu siyo mwandishi wa machafuko, 1 Kor. 14:33. Bwana wetu hakufanya kazi kinyume cha ombi lake la umoja, Yn. 17:20-21. |
| (2) Litaduma milele: Dan. 2:44; Ebr. 12:28-29. | (2) Yatang'olewa: Mat. 15:13. |
| (3) Linajulikana kwa majina ya Biblia: Rum. 16:16; Mdo. 20:28; 1 Kor. 1:2. | (3) Yanatumia majina yalio buniwa na wanadamu, au aina ya serikali, siku, sheria fulani. Lakini ni lazima tuseme kama Mausia ya Mungu, 1 Pet. 4:11. |
| (4) Lilianziswa katika karne la kwanza: Mdo. 2:47. | (4) Katoliki lilianzishwa katika karne ya saba na madhehebu yaliyoanzishwa ili kuwa kinyume cha Katoliki (Protestant) lilianza katika karne ya 16. |
| (5) Mbinguni ni makao makuu: Efe. 1:22, 23; 1 Pet. 3:22. | (5) Makao makuu yao yapo ulimwenguni, Rumi, Independance, Missouri, Cleveland, Tennessee, Brooklyn, New York, na sehemu nyingi tu. |
| (6) Linatumia Biblia tu: Mdo. 2:42; 1 Pet. 4:11; Gal. 1:6-9; Ufu. 22:18-19; Yuda 3. | (6) Yanatumia mapokeo, kanuni, vitabu vya imani, katekisimo, gazeti na vitabu vingine viliandikwa na wanadamu. |
| (7) Tunaongezwa katika Kanisa: Mdo. 2:47. | (7) Tunajiunga kwenye madhehebu: lakini tunaongezwa ndani ya Kanisa, 1 Tim. 3:15. |
| (8) Lazima kwa wokovu: Efe. 5:23; Mdo. 20:28. | (8) Wanadai unaweza kuokolewa bila kuwa mshiriki mwaminifu. |
| (9) Lilinunuliwa pale Kalvari: Mdo. 20:28; Efe. 5:25. | (9) Hakuna mtu alinunua dhehebu yake kwa kutoa damu lake kwa ajili ya watu wote. |
| (10) Mitume walikuwa washiriki wa Kanisa hili: Mdo. 2:41. | (10) Hakuna hata mtume moja alikuwa kwenye madhehebu. |
| (11) Lililochaguliwa na Kristo: Mat. 16:18; Kol. 1:24. | (11) Yamechaguliwa na wanadamu: Zab. 127:1. |
| (12) Tunaingia kwa kuamini, kutubu, kukiri na kuzikwa ndani ya maji: Mdo. 2:36-47; 8:26-40. | (12) Yana sheria nyingi ya kujiunga: piga kura, lipa fedha, imani tu, neema tu, kunyunyiza, kumwagia. Matendo yale yote yalianzishwa na wanadamu. |
| (13) Lilianzishwa Yerusalemu: Zek. 1:16; Isa. 2:1-4; Marko 9:1; Luka 24:46; Mdo. 1:1-4. | (13) Yanaanzishwa kila mahali hapa ulimwenguni, siyo Yerusalemu. |

## Hitimisho:

Kanisa la Agano Jipya halifanani na madhehebu. Na ni lazima leo tusijaribu kufanana na madhehebu kwa sababu tukifanya hivyo tutapotea. Yesu alijenga Kanisa Lake, kuwemo ndani yake.

**Somo La Thelathini Na Moja** **Jina ________________**

# Kanisa la Kristo Sio Dhehebu

(Sehemu ya Nne)

## Sababu Kumi Na Tatu:
## Kwa Nini Kanisa La Kristo Sio Dhehebu.

1. Umadhehebu ni kinyume na Sala ya Bwana katika Yoh. 17:20-21.
2. Umadhehebu ni uasherati wa kiroho, Yoh. 17:20-21.
3. Umadhehebu ni kosa kwa sababu Yesu hajagawanyika, 1 Kor. 1:11-13.
4. Umadhehebu ni kosa kwa sababu Yesu ana mwili moja, sio mingi 1 Kor. 12:13, 20; Efe. 4:4; Kol. 3:15.
5. Umadhehebu unapinga sababu na kusudi ya msalaba, Efe. 2:15-16.
6. Umadhehebu ni kazi ya bure, Mat. 15:9; Zab. 127:1.
7. Umadhehebu unagawanya nyumba za watu, Yoh. 24:15; Amosi 3:3; Marko 3:23.

8. Umadhehebu unapinga ombi la umoja la Paulo, 1 Kor. 1:10.
9. Umadhehebu ni kinyume cha mafundisho ya mitume, Rum. 16:17-18.
10. Umadhehebu ni dhambi ambayo Mungu hapendi, Mith. 6:6-19.
11. Umadhehebu inaonyesha Mungu ni mwandishi wa machafuko, 1 Kor. 14:33.
12. Umadhehebu siyo wa mitume.
13. Umadhehebu itahukumiwa, Marko 3:24-25.

## Dawa Ya Kupona Madhehebu

Kama hatutaki umadhehebu ulendelee tunahitaji wote kurudi kwenye maandiko. Tuache katekismo, kanuni, mawazo ya wanadamu na kufuata kitabu cha Mungu. Leo kama wapo watu wanabishana kwa sababu hawajui saa ngapi. Wakitafuta saa basi watajua muda. Kwa hiyo leo kama tunabishana kuhusu dini ni lazima turudi kwenye Biblia. Biblia tu ina mamlaka leo na Biblia tu inaokoa. Na kama sisi wote ulimwenguni tutafuata Biblia tu basi tutakuwa na "Umoja wa Roho" Efe. 4:1-6.

Pia ni lazima tujue kwamba mbegu inazaa yenyewe. Mbegu ya nyanya haiwezi kuzaa mahindi, Mwa. 1:12. Kwa hiyo kama tunafuata Mbegu ya Neno, Lk. 8:11, hatuwezi kukosa kuwa Kanisa la Agano Jipya. Kwa sababu mbegu ya Neno inazaa Wakristo tu!

Kanisa la Kristo sio dhehebu. Bwana wetu alikuwa bila dhehebu na anatuomba tuwe na umoja katika maneno yake. Kwa hiyo wakati Yesu aliomba kwa Baba yake katika Yoh. 17, alijua tunaweza kuwa na umoja kama tutafuata maneno ya Baba yake. Kwa hiyo kama watu wa Madhehebu wanataka kuponywa leo, ni lazima waache mafundisho yao na kushika maandiko tu!

**Maswali:**

1. Fafanua neno "Dhehebu" ina maana gani?

2. Toa mifano kutoka Agano Jipya yanayoeleza umoja wa Kanisa.

3. Taja sababu zinzoaeleza Kanisa la Yesu sio Dhehebu.

4. Madhehebu yanatakiwa kufanya nini kama yanataka kuabudu kama mitume walivyoabudu?